



UFAPANUZI KUHUSU TANGAZO LA UHAKIKI WA MAKAMPUNI

Hivi karibuni Ofisi yetu ilitoa Tangazo linalowataka wote wenye kampuni Tanzania kuleta Taarifa za Kampuni zao kwa nia ya ofisi yetu kufanya tathmini ya zile ambazo bado zinafanya shughuli na ambazo zimeacha kufanya shughuli zake.

Tunapenda kuwafahamisha tena kwamba taarifa hizo zinazoletwa kwa Msajili zinapaswa pia kueleza kama kampuni husika imekuwa na bado inawasilisha Mizania yake (Annual Returns) kwa Msajili, kila mwaka kama sheria inavyotaka.

Tunapenda pia kutoa shukuruani kwa wale ambao tayari wamekwisha leta taarifa zao tukiwaomba nao watutaarifu tena kuhusu hali ya uwasilishaji Mizania ya Kampuni zao.

Kwa ufapanuzi huu basi tunaomba taarifa hizo zitakazokuja sasa zije na maelezo haya kuhusu uwasilishaji wa Mizania hiyo.

Sambamba na maelezo hayo, wale ambao walikuwa hawawasilishi hiyo Mizania, watatakiwa sasa kufanya hivyo mara moja ili kuepusha Kampuni zao kufutwa.

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaokuwa umejitokeza.

MSAJILI WA MAKAMPUNI